
Editon Consortium Journal of Kiswahili [ISSN: 2663 - 9289]




**Issue no:** 1 | **Vol no:** 5 | **August** 2024: 21-31

# Utambulishaji wa mada za kigaidi katika diskosi ya ugaidi katika magazeti teule ya Kenya na ya kimataifa

**Gichohi M.Kiguta** [(1)]
**Ogola J. Onyango** [(2)]
**Wandera S. Simwa** [(3)]

(1.2.3) Chuo Kikuu cha Laikipia, Kenya.
Main author email: **mchlkiguta@yahoo.com**

**Article History**
Received: 2024-06-02
Accepted: 2024-07-08
Published: 2024-08-23

**Cite this article in APA**
Kiguta, G. M., Onyango, O. J., & Simwa, W. S. (2024). Utambulishaji wa mada za kigaidi katika diskosi ya ugaidi katika magazeti teule ya Kenya na ya kimataifa. *Editon consortium journal of Kiswahili*, *5*(1), 21-31. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v5i1.522

**Ikisiri**
Utafiti huu ulilenga kutambua mada mbalimbali zilizojitokeza katika mashambulizi ya kigaidi na kuripotiwa na wanahabari wa Kenya na wa Kimataifa katika mashambulizi ya kigaidi nchini Kenya kati ya mwaka wa 2013- 2015. Sababu kuu ya kuteua kipindi hiki ni kutokana mashambulizi makuu nchini Kenya yaliyosababishwa na kundi la Al-Shabaab dhidi ya serikali ya Kenya. Mashambulizi mawili makuu yaliyotekelezwa nchini Kenya yalikuwa ni ya Westgate mjini Nairobi na katika Chuo Kikuu cha Garissa. Ili kupata data ya uchanganuzi kuhusu mada za kigaidi, magazeti mawili makuu nchini Kenya yaliteuliwa ambayo ni Daily Nation na The Standard. Gazeti la New York Times liliteuliwa kutokana na mkabala wa jukwaa la kimataifa. Jumla ya magazeti 145 yalikusanywa na nakala 102 kuteuliwa. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Ubishi iliyojikita katika nadharia ya Pragmadeiletiki ya mhakiki ubishi Houtlousser na Frans Van Eemeren. Uchanganuzi huu wa ubishi ulipitia vitengo vya kipragmatiki. Mada za kidiskosi zilihusu, ufisadi, utetezi wa haki za kibinadamu, umoja na utangamano, umwagikaji wa damu, athari za matokeo ya vita, ulipizaji kisasi, uzalendo, nafasi ya vijana katika jamii na usalama. Matokeo ya utafiti huu yalibainisha ya kuwa kulikuwepo na tofauti za kimkabala kati ya kundi la kigaidi dhidi ya serikali ya Kenya. Ilipendekezwa kuwa mada za kigaidi katika eneo la kimataifa kama vile mashambulizi ya ugaidi kati ya Waisraeli na vita vya Gaza zinastahili kutiliwa maanani katika tafiti zijazo kwa kuwa matokeo yake yangeliweza kuwa mchango mkubwa katika kuendeleza utafiti wa diskosi za kisiasa.

**Maneno muhimu**: Kimataifa, mada, magazeti, siasa, ugaidi.

Editon OPEN ACCESS

This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines. The work without further permission provided the original work is attributed as specified on the SAGE and Open Access pages

**UTANGULIZI**

Diskosi ya ugaidi imeendelea kuwa swala sugu katika kila pembe ya ulimwengu. Hii ni kutokana magaidi ambao wameendelea kuzua hofu, vitisho, woga na vifo kwa wanajamii. Ni bayana kuwa ugaidi umeendelea kuwa na mitazamo tofauti ya kimkabala, kimkakati na kimatumizi. Tofauti hizi ni kati ya makundi ya kijamii yanayolumbana katika mgogoro wa ubishi ambapo kila kundi hutambulisha mwenzake kupitia mtazamo wa msimamo uliojikita kwenye itikadi.

Mada inayohusu ugaidi huwa yenye uchangamano na utata mkubwa (Schmid, 2004). Mada za kigaidi huzua msisimuko mkubwa katika hisia za kibinadamu kila zinapojadiliwa (Jowett & O'Donell, 2006). Mada hizi huambatana na maswala mengi yanayoathiri jamii kama vile ya kisiasa, kisaikolojia, kiusalama na kihistoria (Goodin, 2006). Mbali na kuatua mioyo ya wanajamii ugaidi hutumia mikakati ya kihalifu kupitia mashambulizi yanayonuia kutishia usalama wa wanajamii (Cole, 2003). Schmid (2004) anaeleza kuwa ugaidi ni mkakati unaotumiwa na makundi ya kijamii kupasha habari kwa mtu au watu wanaodhamiriwa kuwa ni maadui kwa kutumia mbinu za kuogopesha kwa kauli ya kuwa, 'Mtu mmoja afe ili maelfu ya watu waweze kuhofia na kuogopa'. Muktadha wa ugaidi huhusisha mashambulizi ya ugaidi dhidi ya serikali na raia wasiokuwa na hatia (Exposito, 2002). Ugaidi umesababisha ubishi mkubwa wa kimkabala unaobainika kupitia mkakati wa utendaji, wa lugha na itikadi (Armstrong, 2000).

Imani ya dini imetumiwa na baadhi ya makundi ya kigaidi kama mkakati wa ubishi kuzua vurugu na kusababisha hasara dhidi ya serikali na mataifa mbalimbali ya dunia (Rusel & Tyler, 2010). Baadhi ya makundi ya kigaidi ambayo hutumia dini kama mkakati wa mapambano ni Al-Qaeda, Al-Shabaab na Boko Haram (Ross, 2006). Dini ya Islamu imetumiwa na baadhi ya makundi ya kigaidi kuhalalisha mashambulizi kupitia sehemu teule za maandiko, (Jackson, 2005). Nchini Kenya, ubishi katika diskosi ya ugaidi ulibainika kupitia kundi la Al-Shabaab dhidi ya serikali ya Kenya na ya kimataifa katika mashambulizi ya Westgate (2013) na Chuo kikuu cha Garissa (2015).Ni kutokana na tofauti hizi za kimkabala katika makundi ya kijamii iliyopendekeza mtafiti kuhakiki na kuchanganua diskosi hii kwa kina kupitia msingi wa kinadharia. Utafiti huu ulinuia kuliziba pengo hilo la kiusomi. Ugaidi umezua tatizo kubwa ulimwenguni. Swala la ugaidi limeendelea kukita mizizi na kuzua changamoto kutokana na mikakati inayotumiwa ya kusababisha woga na hofu kwa wanajamii (Schmid, 2004). Ugaidi umeendelea kukosesha serikali amani kwa kuvuruga usalama wa nchi (Maria, 2012). Utafiti huu uliteua na kuchunguza mada mbalimbali za kidiskosi zilizoibuka katika mashambulizi ya ugaidi na kurekodiwa na wanahabari wa Kenya na wa Kimataifa. Utafiti huu ulizingatia matukio ya mashambulizi mawili makuu ya ugaidi nchini Kenya ambayo yaliyosababishwa na kundi la Al-Shabaab kati ya kipindi 2013 na 2015. Mashambulizi haya ya kihistoria yalihusu: mauaji, uharibifu, uporomoshaji majumba na vitisho.Vyombo vya habari vilitumiwa kupasha habari kupitia wanahabari wa Kenya na kimataifa. Nchini Kenya, magazeti maarufu yaliyoripoti habari za ugaidi yalikuwa ni Daily Nation na The Standard na yalifuatiliwa na mamilioni ya wasomaji wengi nchini Kenya na Afrika Mashariki na kwa hiyo yalikuwa muhimu katika kujenga maoni na mkabala wa wasomaji (Chouliaraki, 2001). Gazeti la New York Times liliteuliwa kutokana na mtazamo mpana kuhusu mada za ugaidi katika jukwaa la kimataifa (Malashenko 2017). Gazeti la New York Times mbali na kuwa na ushawishi mkubwa kuhusu mkabala wa kimataifa lilikuwa na nguvu ya kuonyesha msimamo wake dhidi ya ugaidi (Van Dijk, 2008).

Utafiti huu ulijikita katika magazeti ya kipindi cha kihistoria kuhusu mashambulizi ya Al- Shabaab kati ya mwanzoni mwa 2013 na mwishoni mwa 2015 kuhusu mashambulio ya Westgate mjini Nairobi (2013) na Chuo kikuu cha Garissa (2015). Data zinazohusu mada mbalimbali za matukio ya ugaidi zilizokusanywa maktabani na kulezewa kwa kirefu kupitia mkabala wa mtazamo wa makundi mawili ya kijamii yaliyokuwa katika mapambano. Fairclough (1989) anaeleza kuwa vyombo vya habari kama vile magazeti yalikuwa na uwezo wa kushawishi wasomaji kufuata mkabala dhidi ya magaidi. Magazeti ya Kenya na ya kimataifa yaliweza

kuelezea habari za matukio ya kigaidi kupitia mtazamo wa serekali na waandishi wa habari (Van Dijk, 1976). Katika usomaji wa magazeti, hadhira ilihakiki muktadha wa yaliyomo kuhusu diskosi ya ugaidi kutokana na tajriba yao imani na maadili (Halliday, 1978).

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Ugaidi husababisha madhara kama vile ya kupanda kwa gharama ya maisha, matatizo ya kiakili, woga na wasiwasi, ukosefu wa usalama, maisha ya fedheha, ulemavu, fikra za kujichukia, unyanyapaa ,kutamauka maishani, hasira, hisia za maonevu , kudharauliwa pamoja na hisia za ukosefu wa haki za kibinadamu (Hoffman, 2006). Magaidi walitumia mapigano ya kivita ili kulazimisha serikali ikubali itikadi na mtazamo wake wa kimkabala walioupendekeza (Ali, 2008). Mbinu ambazo magaidi walitumia zilihusu utoaji vurugu, uvamizi na mashambuliaji kwa raia, uharibifu wa mali na rasilmali pamoja na kulenga wakuu wa kiserikali (Cohen, 2009). Mkakati mwingine ulitumiwa na magaidi kushurutisha serikali kukubali madai yake ulikuwa ni: ujitoaji uhai, ulipuaji wa mabomu, ushambuliaji kwa silaha kama visu na bunduki, ulipuaji wa mabomu kwa kupitia magari na ulipuaji wa vilipuzi mbalimbali (Schmid,2004). Nchini Kenya, kundi la kigaidi ambalo lilihusishwa na ugaidi lilikuwa ni Al-Shabaab (Taaliu, 2017). Anwar (2009) anaeleza kuwa chimbuko la neno “Al-Shabaab” ni la Kiarabu, ambalo ni ‘Harakat al Shabab al –Mujaheedin’-HSM, lililomaanisha kundi la vijana la Kisomali la kiharakati la Ki- Jihad au Mujaheedin.

Kundi la Al-Shabaab huwa linaloongozwa na itikadi kali zinazofungamana na sheria ya imani ya uislamu (Schmid, 2004). Mojawapo ya itikadi inayozingatiwa na kundi hili ni upigaji marufuku wa muziki wa burudani na unyoaji ndevu kwa wanaume (Odhiambo, 2014). Al-Shabaab ni zao la kundi la kigaidi la Al-Qaeda na limekuwa likiendeleza itikadi iliyotolewa na kundi la Al-Qaeda kupambana na mataifa makubwa duniani (Hansen, 2013). Makundi haya mawili ya Al-Qaeda na Al-Shabaab ndiyo yameelekeza mashambulizi yake dhidi ya mataifa yanayoenda kinyume na mkabala unaofungamana na imani zaa itikadi zao (Schmid, 2004; Gartenstein -Ross, 2009).Kundi la Al-Shabaab lilivumbuliwa Somalia kupitia Islamic Courts Union (ICU) mwaka wa 1996 na Ibrahim Haji Jaama’ Al-Afghani (Maria, 2012). Mnamo mwaka wa 2012 kundi hili la Al-Shabaab lilijiunga na Al-Qaeda ambapo wanamgambo wa Al-Shabaab wenye itikadi kali walizindua jeshi la ki-jihad lililokuwa na kikosi cha wanajeshi kati ya 7000-9000 mwaka wa 2014. Idadi kubwa ya kikosi hiki cha Al-Shabaab ilitoka katika nchi ya Yemen, Sudan, Kenya, Tanzania, Afghanistan, Saudi Arabia, Malayasia, Pakistan na Bangladesh (Malashenko, 2017). Ahmed Abdi Godane, komanda na mwanzilishi wa Al-Shabaab alitangaza kuwa Al-Shabaab lilikuwa na uhusiano wa karibu na Al-Qaeda (Lacquer, 2001).Wapiganiaji wa Al-Qaeda waliopata mafunzo yao ya kijeshi kutoka kambi za Afhaghanistan walihamia Somalia kuwapa Al-Shabaab mafunzo ya kivita (Odhiambo, 2014).

Makundi ya Al-Qaeda na Al-Shabaab yaliendelea kushirikiana na kupokezana mafunzo ya utumizi wa vilipuzi vya mabomu na mauaji ya ujitoleaji uhai pamoja na utekaji nyara. Kati ya wapiganaji 3,000 hadi 5,000 wa kivita na zaidi ya vijana 200 hadi 300 hawakuwa raia wa kutoka Somali bali walitoka nchi za nje (Jackson, 2005). Vijana wengi katika kundi la Al-Shabaab walikuwa wametoka katika maeneo mengine ya Bara la Afrika (Norris et al., 2003).Mnamo Septemba 2014, Godane aliuawa kupitia ndege ya roboti kutoka jeshi la Marekani (Odhiambo, 2014). Tangu kifo chake viongozi wa nchi ya Somali walikuwa wakiishi kwa tahadhari ili Al-Shabaab isije kuwashabulia raia wa kisomali kwa kulipiza kisasi kutokana na sababu ya kuwa Al-Shabaab lilikuwa ni maadui wa taifa la Somalia (Martin, 2003). Lengo la kundi la Al-shabaab kama lilivyokuwa kundi la Al-Qaeda lilikuwa ni kulenga shabaha yake kwa mataifa waliyoyaona kama maadui zao, (Martin, 2008). Mkakati waliotumia kushinikiza mataifa waliodai kuwa ni wakinzani wao ulikuwa ni kuvamia raia wanyonge wasiokuwa na hatia. Mbinu nyingine waliotumia ilikuwa ni kusababisha hasara ya mali na rasilmali kwa kuporomosha majumba ya kiutawala na kuvamia viongozi. Makundi haya ya magaidi yalianzisha hoja za ubishi mkali zilizojikita katika itikadi na msimamo (Hansen, 2013). Mbinu zingine

zilizoanzishwa na makundi katika mapambano ya ugaidi yalihusu propaganda na upotoshi katika ukuzaji wa mgogoro,(Oando & Achieng, 2021)

Exposito (2002) anaeleza kuwa mtazamo wa kundi la Al-Shabaab dhidi ya serikali ya Kenya ulikuwa wa ubaguzi. Lilidai kuwa seriekali ya Kenya ilikuwa ikiingilia maslahi ya kindani ya Somalia huku ikijifanya kulinda usalama wa raia wake, (Kimotho, 2019). Ili kuishinikiza Kenya iyaondoe majeshi yake nchini Somalia, Al-Shabaab lilianza kuyashambulia maeneo mbalimbali ya Kenya (Odhiambo, 2014). Mkakati mojawapo wa kigaidi ulioendelezwa na Al-Shabab ulihusu kuyalipua majengo makubwa na sehemu zilizokuwa na kusanyiko kubwa la halaiki ya watu. Kundi la Al-Shabaab lilidai kuwa nchi ya Kenya ilikuwa ikiuka sheria zilizowekwa na shirika la dunia kuhusu haki za kibinadamu kwa kuwapeleka majeshi yake kuvamia nchini Somalia kwa madai ya kulinda amani. Kinaya kilichojitokeza ni kuwa kundi la Al-Shabaab lilijiwakilisha kama kundi la wanyonge linalodhulumiwa na taifa kubwa la Kenya, kwa hivyo lilitaka lihurumiwe na mataifa mengine ulimwenguni, (Maria, 2012). Kundi la Al-Shabaab lililaumu serikali ya Kenya kuwa ilikuwa ikifadhiliwa na kuungwa mkono na taifa la Marekani ambalo kwao waliliona kuwa ndilo lililokuwa "adui mkubwa wa kigaidi duniani" (Michael & Lars, 2010).

Al-Shabaab lilichukulia mkabala wa kuwa lilikuwa likibaguliwa na mataifa ya Kenya na Marekani kupitia mtazamo wake wa kiitikadi, kidini na kimwelekeo. Jambo ambalo lililosababisha kundi hilo kuanzisha vita vya ulipizaji kisasi (Fischer, 2004; Cohen, 2009). Jambo kuu lililosababisha kundi la Al-Shabaab kuchipuka lilikutokana na mabaki ya wafuasi wa kundi la Al-Qaeda ambalo lilikuwa limepokea mafunzo yake ya kivita kutoka kwa kundi la Al-Itihaad Al-Islamiya (AIAI). ) nchini Somalia, (Friendlander, 1976). Al-Shabaab lilichukua usukani wa kuendeleza kundi hilo la Al-Ittihaad baada ya maanguko ya serikali ya Somalia mwaka wa 1991. Kundi la Al-Itihaad Al-Islamiya liliundwa kwa madhumuni ya kulazimisha sheria ya Uislam ("Shariah law"), lakini nchi ya Uhabeshi ilijihami kutokana na maendeleo ya wanajamii wa Islami, Wahhabi na Salafi ambao waliokuwa wakijitokeza kuwa wangekuja kuwa tishio kubwa kwa wakristo (Michael & Lars, 2010). Jeshi la Wahabeshi lilivamia Somalia na kuyaharibu makundi ya Al-Itihaad Al-Islamiya na Muungano wa Mahakama za Kiislam (ICU) mwaka wa 2004 na 2006 kabla hayajatawanyika na kuongezeka (Michael & Lars, 2010). Al-Shabaab ilibaki kuwa miongoni mwa makundi ya kigaidi yaliyosalia baada ya kundi la Al-Itihaad Al-Islamiya kusambaratika na kutoweka (Walzer, 2004). Kundi la Al-Shabaab lilijiimarisha na kukua kwa haraka sana katika maeneo ya Somalia na Kaskazini mwa Kenya, (Cole, 2013). Kundi la Al-Shabaab ni zao la watu ambao walijitoa mhanga kupigania matakwa na maslahi yao ya jamii zao kiitikadi kwa kutumia vitisho na mashambulizi kwa raia kwa malengo ya kisiasa (Hansen, 2013). Mkabala wa Al-Shabaab ulikuwa na itikadi ya kuwa lilikuwa linabaguliwa na mataifa yaliyokuwa na nguvu kisiasa, kiuchumi, kijeshi na kiutawala na kwa hiyo halikuwa na budi ila kulipiza kisasa kujikomboa dhidi ya maonevu (Toomey & Singleton, 2014). Vita vya kigaidi dhidi ya taifa la Kenya vilihusu kulenga kudhoofisha serikali katika sekta muhimu za kitawala kama vile za taasisi za kiuchumi, kitaalii, kiusalama na kimawasiliano (Hansen, 2013).

Kundi la Al-Shabaab lilikuwa na mtazamao wa kuwa taifa la Marekani lilikuwa likifadhili na kulipa msaada taifa la Kenya kifedha na kijeshi. Al-Shabaab lilidai kuwa ni kutokana na kuisaidia taifa la Kenya ndipo majeshi ya Kenya yaliweza kushambulia maeneo ya Somalia . Ili kujikomboa na dhuluma za mataifa kinzani kama vile Kenya na mataifa mengine Al-Shabaab ilibuni mkakati wa vita vya mashambulizi ya kighafla (Schmid, 2004). Mojawapo ya mbinu ambazo zilizotumiwa na Al-Shabaab ilikuwa ni kuzua hofu na woga kwa wanajamii kwa kusababisha vurugu ya mashambulizi, (Odhiambo et al., 2013). Mbinu nyingine ya kivita ilikuwa ni kutumia mikakati ya lugha katika mgogoro wa ubishi kwa njia ya propaganda, utiliaji chuku, na upotoshi kama silaha ya malumbano dhidi ya Kenya na nchi zingine za kimataifa (Lacquer, 2001).

Vyombo vya habari vilichukua nafasi kubwa katika propaganda ambapo Al-Shabaab ilivitumia kama

jukwaa la kupazia sauti kwa kutolea matangazo ya vitisho, kurekodi matukio na kusambaza woga zaidi kwa wanajamii (Ross, 2006; Reah, 2002; Igwebuke, 2018). Kundi la Al-Shabaab lilitumia itikadi ya imani ya dini ya uislamu kuhalahalisha tendo lake la kuwa lilikuwa ni maelekezo yaliyotoka mbinguni na pia ahadi ya Mungu (Ali, 2008; Akwiri, 2014). Kundi la Al-Shabaab lilijipa haki na nguvu ya kuendeleza mashambulizi yake huku ikiendeleza ikitoa mafunzo ya kivita kupitia maandiko kutoka Koran, (Anwar, 2009). Dini ya uislamu ilitumiwa kama silaha ya kujikinga na kujidhibiti dhidi ya serikali ya Kenya (Ross, 2006). Lengo kuu la Al-Shabaab lilikuwa ni kulifanya eneo nzima la Afrika Mashariki liwe Khalifa ya himaya ya Uislamu (Maria, 2012). Ahmad na Azzam (1976) wanaeleza kuwa kundi la Al-Shabaab liliongozwa na dai la 'ki-jihad' lililomaanisha vita vitakatifu vya waumini wa kiislamu na ukombozi wa waislamu kwa kushambulia yeyote aliyekuwa ni 'kafiri' au asiyekuwa mwislamu,(Maria, 2012).

Kundi la Al-Shabaab liliteua baadhi ya maneno ya korani kwa hila na kuyafanya yaonekane kuwa ya kweli kwa lengo la kuamsha hisia za ghadhabu za chini kwa chini kwa wafuasi wao (Jackson et al., 2009). Mkakati wa matumizi ya propaganda kupitia maandishi ya dini ya Islamu ulikuwa muhimu kujenga hisia kali za kiitikadi na chuki katika ubishi, (Norris et al., 2003). Propaganda ilikuwa muhimu kama mkakati wa kujikuza na kuenezea uvumi kuwa kundi la Al-Shabaab lilikuwa ni kundi kubwa lililopaswa kuogopewa kutokana na uwezo mkubwa wa kivita lililokuwa nao. Propaganda ilitumiwa kushawishi mashirika ya udumishaji amani ulimwenguni kuliunga mkono Al-Shabaab kwa madai ya kudhulumiwa na mataifa makubwa kama vile Kenya na Marekani. Al-Shabaab lilitaka taifa la Kenya liyaondoe majeshi yake ya KDF pamoja na ya umoja wa shirikisho la kupigana na magaidi Afrika, (AMISON) kutoka maeneo ya Somalia (Ditrych, 2014).

Raia wa Uingereza nchini Kenya wamekuwa wakiandamwa na magaidi hata kutekwa nyara (Martin, 2008). Mashambulizi ya kigaidi yamekuwa yakizuka ghafla bila kutarajiwa wakati wowote hasa nyakati kunapokuwa na likizo za sherehe za kidini kama vile iddul-fitr (Martin, 2003, 2008). Matendo ya Al-Shabaab yamesababisha kundi hili kuhesabiwa miongoni mwa makundi makubwa ya ugaidi duniani (Akwiri, 2014). Kundi la Al-Shabaab ndilo lenye tishio kubwa zaidi nchini Kenya kutokana na itikadi ya misimamo mikali iliyojikita kwenye dini ya islamu, (Ahmad, 1977). Kundi la Al-Shabaab hudai kupigania haki dhidi ya serikali ya Somalia na raia wake. Mnamo Januari 8, 2020, kundi la Al-Shabaab lilitoa tangazo la tishio lilinalolenga serikali na raia wa Kenya, (Michael & Lars, 2010). Kundi hili lilidai kuwa serikali ya Kenya ilikuwa ikiingilia maslahi yake ya ndani kwa kutuma majeshi yake nchini Somali kudumisha amani (Taaliu, 2017). Kutokana na mtazamo wa kundi la Al-Shabaab nchi ya Kenya ilikuwa ikitumia mbinu za ulaghai na propaganda kudhulumu raia wake huku ikijisingizia kulinda usalama katika nchi ya Somalia, (Ross, 2006).

Hali hii ilisababisha Al-Shabaab kuendeleza msururu wa mashambulizi dhidi ya Kenya (Maria, 2012). Kwa upande wake serikali ya Kenya ilijibidiisha kujaribu kupambana na ugaidi kwa kuimarisha vikosi vya ulindaji usalama ndani na nje ya mipaka yake. Michael na Lars, (2010) wanaeleza kuwa kuna ushahidi wa kutosha kuwa kundi la Al-Shabaab lilikuwa likifadhiliwa na na kundi la kigaidi la Daesh ambalo (awali lillijulikana kwa jina la ISIL), ili kutekeleza mashambulizi dhidi ya Kenya. Kundi la Daesh lilifanya Al-Shaabab liendeleze msururu wa mashambulizi nchini Kenya. Mnamo tarehe 15 hadi 16, Januari, 2019, kulitokea mashambulizi ya ugaidi katika mkahawa wa kibiashara wa Al-Dusit maeneo ya Riverside mjini Nairobi ambapo raia wa Kenya walijeruhiwa na kuuawa. Raia mmoja wa taifa la Uingereza aliuwawa kutokana na mashambulizi hayo (Malashenko, 2017). Mnamo tarehe 2 Aprili, 2, 2015, kulizuka shambulizi la kigaidi katika Chuo kikuu cha Garissa ambapo raia wa Kenya wapatao 148 waliuawa (Jackson, 2016). Kati ya mwezi wa Juni na Julai, 2014 shambulizi la kigaidi lilizuka katika kaunti ya Lamu na mto Tana na maeneo ya pwani mwa Kenya ambapo raia 85 waliuawa (Kimotho, 2019). Mnamo Kati ya Septemba 21 -24, 2013, raia wa Kenya zaidi ya wakenya 60 pamoja na raia wengine 6 kutoka Uingereza waliuawa kwenye duka la kibiashara la Westgate mjini Nairobi (Odhiambo, 2014). Kumekuwa na mashambulizi

mengine mengi yaliyohusishwa na Al-Shabaab mpakani mwa Kenya hasa katika maeneo ya Kaskazini Mashariki, (katika kaunti za Lamu, Garissa, Wajir na Mandera. Hali hii ilielekeza serikali ya Kenya kuongezea majeshi ya KDF katika maeneo ya msitu wa Boni na mpakani mwa Kenya na Somalia ambapo makundi ya Al-Shabaab yalikuwa yamekolea (Michael & Lars, 2010). Majengo makuu ya kiserikali na kambi za ulindaji wa usalama zilikuwa zikilengwa na makundi ya kigaidi (Martin, 2008). Masilahi ya serikali ya Somali nchini Kenya pia yamekuwa shabaha inayolengwa na magaidi (Norris et al., 2003).

Kila kunapotokea mashambulizi ya kigaidi wanahabari hufika haraka katika maeneo hayo ili kupata habari za moja kwa moja zinazowasilishwa haraka kwa hadhira (Bednarek, 2006). Wanahabari hutoa maelezo ya matangazo ya visa walivyoshuhudiwa vya kigaidi kwa wanajamii kwa kurekodi maandishi na kupigaji picha na filamu (Schmid, 2008). Kwa kuwa wanahabari ni kiungo mojawapo cha wanajamii, huandika mambo yanayohusu jamii zao kulingana na mkabala wa mwonoulimwengu wa mazingira ya jamii zao, (Van Dijk, 1988; Chouliaraki, 1999; Reah, 2002). Wanahabari hujipata wakielezea habari walizoshuhudia na kutawaliwa na hisia, mielekeo na maoni yanayotokana na mkabala wa itikadi za serikali zao. Makundi ya kigaidi yalifahamu umuhimu wa upashaji habari kufikia halaiki kubwa ya wanajamii kupitia vyombo mbalimbali vya habari kama vile magazeti (Rusell & Tyler, 2010). Diskosi ya ugaidi kupitia upashaji wa habari zilionyesha jinsi kiwango kikubwa cha vurugu kilivyotokea, jambo ambalo liliwezesha kusaidia magaidi kuzidisha hofu kwa wanajamii (Toomey & Singleton, 2014). Fairclough (1995) anaeleza kuwa watangazaji wa habari walikuwa wakitumiwa na magaidi kuwapa sifa za kuogopewa na za kishujaa bila wao kufahamu kuwa hadhira walikuwa wakiwatukuza.

Magaidi walifahamu kuwa wanahabari walitaka kutangaza habari zilizovuma na zilizoweza kufikia soko kubwa la halaiki ya watu na walitumia nafasi hii kusambaza matukio ya matendo yao (Richardson, 2005). Huu ulikuwa ni mfumo wa mkakati mpya uliotumiwa na magaidi wa kushambulia maeneo fulani na kufahamisha wanahabari kuhusu matukio ya kigaidi yaliyoibuka, (Reah, 2002). Kwa njia hii magaidi kupitia vyombo vya habari waliweza kukuza na kuonyesha hasara kubwa iliyotokana na matendo ya itikadi zao (Reah, 2002). Kwa kutumia mbinu ya propaganda, magaidi walifafanua na kujikuza, kutishia na kuafafanulia matendo yao kuwa waliweza kusababisha hasara kubwa kwa wanajamii, (Maria, 2012). Magaidi walitumia mkakati wa matumizi ya upotoshi na chuku zilizoandama na matendo yao ili kulishinikiza taifa la Kenya kuzingatia madai yake. Mbinu zingine zilizotumiwa na magaidi kupitia vyombo vya habari ni utiliaji chuku na upotoshi (Schmid, 2008). Mkakati huu uliyawezesha makundi ya magaidi kuishinikiza raia na serikali kutafuta njia zifaazo za upatanishi dhidi ya madai yaliyotolewa (Benhaddou, 2021).

Upashaji wa habari uliwapa magaidi sifa za ujasiri wa na kijagina kuwa kundi ndogo liliweza kudhibiti na kutatiza serikali zilizokuwa na uwezo mkubwa wa kiutawala, kijeshi na kifedha (Norris et al, 2003). Kundi la Al-Shabaab lilidai kuwa ndilo lililohusika na utekelezaji wa mashambulizi dhidi ya serikali ya Kenya (Walton, 2013). Al-Shabaab lilijigamba kupitia kwa vyombo vya habari kuwa lilikuwa na uwezo mkubwa wa 'kushambulia na kuyashinda maadui yake', (Daily Nation, 2013). Kundi la Al-Shabaab lilitenda mashambulizi ya ugaidi kimaksudi na kusherehekea ushindi wao (Schmid, 2004).

Marekani ndiyo iliyokuza kundi la Al-Qaeda (Malashenko, 2017). Ni katika mwaka wa 1998 ndipo shambulizi kubwa zaidi la mapambano dhidi ya wanajamii liliwahi kuonekana na kushuhudiwa nchini Kenya. Shambulizi hilo lilisababishwa na kundi la Al-Qaeda ambapo jumba la kibalozi la Merikani lilipuliwa (Gartenstein, 2011). Shambulio la New York mjini Marekani lililosababishwa na Al-Qaeda ndilo limewahi kuwa kubwa ulimwenguni. Shambulizi hilo lilitendeka mnamo Septemba 11, 2001 (Exposito, 2002). Majumba manne makubwa yaliteketezwa na kusababisha hasara kubwa ya kiuchumi na usalama wa kijamii. Wakati uo huo Jengo la kaskazini la World Trade Centre liliporomoshwa na mengine kulipuliwa. Takwimu za shirika la Global Data Base (2019), zilionyesha kuwa takriban watu 2602 na wengine 125 walipoteza

maisha yao wakati ndege ya kigaidi ilitumiwa na magaidi kuangusha jumba la Pentagon (Exposito, 2002). Oando na Achieng (2021) walieleza kuwa kutokana na mashambulizi hayo mwamko mpya ulizunduliwa wa kupambana na vita dhidi ya ugaidi duniani.

Mataifa ya kimagharibi yalianza kutangaza vita dhidi ya ugaidi na yakachagua Kenya kama mojawapo ya nchi ambazo zingekuwa katika mstari wa mbele katika kupambana na vita dhidi ya ugaidi (Maria, 2012). Mataifa haya ya kimagharibi yamekuwa yakijitolea mhanga kuimarisha usalama nchini Kenya dhidi ya ugaidi kupitia kwa shirika la (Global War on Terror (GWOT) 2001; Hansen, 2013). Habari za ugaidi zilikuwa za kuatua moyo kwa hadhira na zilivuma na kusambazwa kupitia vyombo vya habari duniani kote. Mkakati wa kutenda mashambulizi na kukimbia haraka kujitangaza kwa propaganda kwenye vyombo vya habari kwa kudai kuwa wao ndio waliosababisha mashambulizi ilikuwa ni mbinu iliyofaidi makundi ya kigaidi (Cole, 2003).

**MATOKEO**

Kupitia msingi wa toposi (Lawyer et al., 2014) mada za ugaidi zilidhihirika kutokana na mashambulizi ya kigaidi yaliyotendeka nchini Kenya katika mashambulizi mawili makuu yaliyotumiwa kama sampuli ya mashambulizi ya ugaidi. Mashambulizi haya yalifanyika katika jumba la kibiashara la Westgate mjini Nairobi (2013) na katika Chuo kikuu cha Garissa (2015). Mada 18 ziliteuliwa kutoka kwa magazeti ya Daily Nation, The Standard na NewYork Times kuhusu ugaidi uliosababishwa na kundi la Al-Shabaab dhidi ya serikali ya Kenya. Mada zilizoteuliwa na kuchanganuliwa zilihusu: Ushirikiano, umoja na uzalendo, umwagikaji wa damu na athari za kivita, utetezi wa haki, ulipizaji kisasi, majigambo, udhalimu , nafasi ya vijana katika jamii, usalama, ujitambulishaji uwajibikaji, kifo na mauti, athari ya vita, ukiukaji wa haki, usaliti, tamaa na ubinafsi, migomo na maadamano, utamaushi na uharibifu wa mazingira.

Mada kuhusu ushirikiano, umoja na uzalendo zilidhihirika kupitia wakuu wa serikali kuwahimiza wanajamii wajitoe mhanga kuungana kwa pamoja kwa wito wa kizalendo kupambana na ugaidi. Mataifa ya kimagharibi yaliomba nchi ya Kenya kushirikiana nayo katika kupambana na vita dhidi ya ugaidi kwa kuifadhili nchi ya Kenya kifedha na kupitia mafunzo ya kijeshi. Nchi za kimataifa kama vile Marekani, Japani na Ulaya ziliitaka serikali ya Kenya iimarishe uhusiano wao wa kupambana na vita dhidi ya Al-Shabaab. Katika gazeti la New York Times (2014) lilinukuliwa likieleza kuhusu ushirikiano wa Somali na Marekani kuhusu ugaidi na kuwa Maalim Ayman, kiongozi wa kitengo cha Jaysh Ayman wa kundi la Al-Shabaab aliuawa katika operesheni ya jeshi la Somalia kwa ushirikiano na vikosi vya Marekani. Ayman alikuwa akisakwa na Marekani kwa kuhusiana na shambulio la Westgate nchini Kenya.

Serikali ya Kenya iliwaomba walinda usalama washirikiane kwa pamoja kupiga vita ugaidi. Hata hivyo, makundi ya kigaidi pia yalishirikiana kupigana na Kenya kwa kuwa ilikuwa ikishirikiana na mataifa ambayo magaidi walichukulia kama maadui wao. Kundi la Al-Shabaab lilishirikiana na Al-Qaeda kwa kupata ufadhili wa mafunzo, ala za kivita na usaidizi. Kwa kuwa kila kundi lilishirikiana kusaidiana itikadi ya kusaidia na mkabala wa upande wa usaidizi ulizua ubishi kila kundi likiwa na msimamo wake.

Umwagikaji damu na athari za kivita zilibainika kupitia magazeti kutokana na masikitiko na hofu ya maafa ya raia waliowapata wanajamii kutokana na mashambulizi ya ugaidi ya Westgate na Chuo kikuu cha Garissa ambapo raia wengi walipoteza wenzao. Raia wa Kenya walipoteza maisha ya wapendwa wao na kupata matatizo ya kisaikolojia. Mali na rasilmali ziliteketezwa kupitia mabomu yaliyolipuliwa katika majengo ya Westgate. Mashambulizi haya yalisababisha gharama ya vitu kwenda juu nchini na sekta muhimu kama vile utalii, usafiri na uchumi kuathirika. Kundi la Al-Shabaab, lilifurahia ushindi huu kwa kuwa lilikuwa limepata shabaha yake ya kutia hofu wananchi wa Kenya na kutisha ili iwache kuungwa mkono na mataifa kama vile ya Marekani, waisraeli na wengine, (Altheide, 2002).

Majigambo yalidhihirika kupitia magazeti pale ambapo Marekani kupitia katibu wake John Terry

ilijidai kuwa ilikuwa na nguvu na uwezo wa kifedha na kijeshi kupambana na magaidi. Rais Uhuru wa Kenya akihutubia vikosi vya usalama aliieleza kuwa vikosi hivi vikishirikiana kwa pamoja walikuwa na uwezo wa kupambana na kundi la Al-Shabaab na hata kulimaliza. Al-Shabaab kwa upande wake ilijigamba kwa kuweza kutekeleza mashambulizi yaliofaulu dhidi ya serikali ya Kenya kupitia maafa yaliyotekelezwa nchini Kenya katika Westgate na Chuo Kikuu cha Garissa. Kufaulu huko kupitia mkabala wa Al-Shabaab ni kuwa wananchi wengi waliaga dunia, vitisho na hofu ziliongezeka na habari hizi zingeweza kusambaa na kufikia mataifa ya dunia. Vilevile maeneo yaliyoshambuliwa yalikuwa na raia wengi wa kigeni kwa hiyo ulikuwa mkakati wa kusistiza maendeleo ya nchi katika sekta muhimu kama vile utalii, usafiri na uchumi. Mada kuhusu udhalimu, kifo na mauti na athari za kivita zilijadiliwa na magazeti. Ingawa serikali ya Kenya ilichukulia matendo ya kigaidi kama ya kidhalimu kutokana na maafa ya raia wasio kuwa na hatia, pamoja na uharibifu wa mali na rasilmali, Al-Shabaab kwa upande wake ilichukulia serikali ya Kenya na nchi za kimataifa kama Marekani kama wadhalimu kwa kuungana kwa pamoja kuingilia raia wake kwa masingizio ya kulinda amani.

Magazeti yalimnukuu katibu mkuu wa Marekani, John Terry akiwaomba walinda usalama wa serikali ya Kenya kushirikiana na jeshi lake kupambana na magaidi. Akirejelea taswira ya mashambulizi ya kigaidi katika jumba la kibalozi la Marerikani (1998) alitaka kikosi cha Kenya kiimarike na aliahidi kufadhili serikali ya Kenya kwa wa pesa na vifaa vya kisasa vya kijeshi ili kupiza kisasi dhidi ya Al-Shabaab. Terry alikashifu mauaji ya kinyama ya raia wa Kenya na wafanyi kazi kutoka nchi yakewaliokuwa wakiishi Kenya na akaahidi kupambana na vita dhidi ya ugaidi hadi kuwamaliza. Ulipizaji kisasi pia ulibainika wakati Marekani iliitaka serikali ya Kenya kuwakamata washukiwa wa ugaidi na kuwalipizia kisasi kupitia Mkuu wa shirikisho la Muungano wa mataifa ya Marekani, Bw. John Terry kudai haya. Serikali ya Kenya kupitia vikosi vya kijeshi ilishambulia maeneo yaliyokaliwa na Al-Shabaab nchini Somalia.

Al-Shabaab kwa upande wake iliona tendo la Kenya la kutuma jeshi lake la KDF kama maonevu ya watu wake na kwa hiyo ililipiza kisasi kwa kushambulia duka la Westgate na Chuo kikuu cha Garissa kama njia ya ulipizaji kisasi dhidi ya Kenya kwa kuingilia maslahi yake ya kindani. Kwa kuwajeruhi na kuwaua raia wa Kenya, Al-Shabaab ilichukulia kuwa haikuwa ilikipiza kisasi dhidi ya raia bali shabaha ya udhia uliekelezwa kwa serikali na kwa hiyo kuuawa kwa raia ilikuwa bahati mbaya na pia kwa upande mwingine kulitumika kama mkakati wa kuishinikiza serikali iyaondoe majeshi yake nchini Somalia. Taswira za majeruhi na mauaji ya wanafunzi zilitumiwa na wanahabari kusababisha masikitiko ya mashambulizi yaliyotekelezwa na Al-Shabaab.Risala za rambirambi zilitumwa kwa serikali ya Kenya kuhusu majanga ya ugaidi kutoka kwa mataifa yaliyokuwa na mkabala mmoja na Kenya kama vile Merikani na Japani.

Athari zilizotokana na ugaidi zilihusu uharibifu wa mazingira, ukosefu wa usalama na piga kwa uchumi kupitia sekta za utalii na usafiri. Marekani ililalamikia umwagikaji wa damu na uharibifu kwa raia wake tangu mashambulizi ya kigaidi ya 1998 wakati jumba la kibalozi la Marekani liliposhambuliwa. Nayo makundi ya Al-Shabaab yakishirikiana na Al-Qaeda, yaliitaka Kenya iepuke kuingilia kati maswala ya ndani ya kundi la Al-Shabaab na iyaondoe majeshi yake nchini Somalia. Pia makundi haya yalitaka Kenya iepuke kushirikiana na nchi ya Somalia na kuunga mkono majeshi ya AMISON. Al-Shabaab ililipiza kisasi cha kisiasa kupitia mashambulio ya mfululizo kwa serikali ya Kenya na kwa wanajamii ambao hawakuwa waislamu. Majigambo yalibainika wakati serikali ya Kenya na nchi za magharibi zilijisifu kwa kutangaza uwezo wao wa kifedha, kijeshi na utumiaji wa vyombo vya kisasa vya kivita.

Marekani ilijisifu kwa kuwa ilikuwa na nguvu kupitia umoja wa wananchi wa Kenya na Marekani. Kundi la Al-Shabaab lilijisifia uwezo wake kwa kujitambulisha na madai ya kuwa ndilo lilihusika na mashambulio ya kigaidi ya Westgate na kuandamanisha na picha za video zilizotumwa katika vyombo vya habari, kwa hiyo lilijiona kuwa lilikuwa na uwezo mkubwa. Vijana na wanawake walitumiwa

katika mashambulizi ya kigaidi na kundi la Al-Shabaab kwa kujiunga katika mashambulizi. Vijana wa Kenya na Afrika mashariki walijiunga na Al-Shabaab ili kupata ajira na wanawake kutumiwa katika mashambulizi kwa kuwa iliaminika kuwa ni wanaumme wanaojiunga na ugaidi katika mashammbulizi. Ugaidi ulivuruga usalama wa jamii, taifa na mataifa kwa kushambulia wananchi na kuvuruga maendeleo ya nchi ya Kenya na Somalia. Magaidi walizifanya serikali kuonekana kuwa zilikuwa zinashindwa kupambana na magaidi na kwa upande wa magaidi walichukulia kuwa serikali ya Kenya na Somalia pamoja na muungano wa shirikisho la mataifa barani Afrika , AMISON kuwa yalisingizia kuleta amani katika Somalia ilihali ilikuwa ikiwadhulumu raia wa Somali.

Ujitambulishaji ulibainika wakati kundi la Al-Shabaab lilijatambulisha na uislamu na kuwatenga wanajamii wengine wote iliyochukulia kuwa makafiri. Serikali ya Kenya na kimataifa ilichukulia matendo ya Al-Shabaab kama ya ukosefu wa haki za kibinadamu na kuwabagua kwa mipaka ya 'Wao' na 'Sisi'. Hata hivyo, kila kikundi cha upinzani kilimuona mwenzake kama adui. Kenya ilijitambulisha na mataifa mengine yaliyozingatia demokrasia na utendaji wa haki, ingawa Al-Shabaab kwa mtazamo wake ilichukulia matendo ya Kenya kama yasiyo ya kweli na yalijikita katika propaganda, jambo lililofanya Al-Shabaab kuvamia Kenya.

## HITIMISHO NA PENDEKEZO

**Hitimisho**: Data zilizokusanywa zilidhihirisha bayana kuwa lugha kama nyenzo kuu ya mawasiliano ilitumiwa kama mkakati wa kukuza midahalo, kutoa madai, kutumia vitisho, kushawishi na kubembeleza na hata kuzua ubishi uliojikita katika misimamo ya itikadi. Kwa kuwa matumizi ya lugha ni kitendo cha kijamii na kuwa uhusiano baina ya wanajamii huathiri na kuathirika kupitia jinsi wanajamii wanazungumza baina yao. Makundi ya kijamii yalitumia maneno kukashifu, kulaumu, kukaripia, kushawishi, kulalamika, kukataa, kuunga mkono na kupongeza wale waliodhamiria kusema kama njia ya kuenda kitendo kupitia matamshi. John Kerry, katibu mkuu wa Marekani alitoa vitisho vya kupambana na magaidi kupitia magazeti ya Daily nation, The Standard na New York Times. Al-Shabaab kwa upande wake ilitangaza fatwa na jihadi ya kutekeleza mauaji dhidi ya raia na wakristo katika shambulizi la Westgate (2013).

**Pendekezo**: Ilipendekezwa kuwa mada za kigaidi katika eneo la kimataifa kama vile mashambulizi ya ugaidi kati ya Waisraeli na vita vya Gaza kati ya Waisreli na Wapalestina (Hamas), vita vya Urusi dhidi ya Ukraine, itikadi ya dini na mielekeo na kasumba za mauaji ya ugaidi katika Shakahola japo muhimu zinastahili kutiliwa maanani katika tafiti zijazo kwa kuwa matokeo yake yanaweza kuzua mchango mkubwa wa utafiti katika diskosi ya ugaidi.

## MAREJELEO


Akwiri, J. (2014). *Grenade Attack on Police Vehicle Wounds Two in Kenya's Mombasa*. ReliefWeb. https://reliefweb.int/report/kenya/grenade-attack-police-vehicle-wounds-two-kenyas-mombasa

Ali, A. M. (2008). *The Al-Shabaab Al-Mujahidiin–A Profile of the First Somali Terrorist Organisation.* https://www.files.ethz.ch/isn/55851/AlShabaab.pdf

Anwar, T. B. (2009). *The Language of Terrorism: Al-Jazeera and the Framing of Terrorism Discourse.* Georgetown University.

Armstrong, K. (2000). *The Battle for God: Fundamentalism in Judaism, Christianity and Islam*. HarperCollins.

Bednarek, M. (2006). *Evaluation in Media Discourse: Analysis of a Newspaper Corpus*. Bloomsbury Publishing Plc.

Benhaddou, M. (2021). A Critical Analysis on the Representation of Muslims in Britain in the Daily Mail Newspaper: Applying Discourse Analysis. *International Journal of Language and Literary Studies*, *2*(3), 216–224. https://doi.org/10.36892/ijlls.v2i3.624

Chouliaraki, L. (1999). Media Discourse and National Identity*: Death and Myth in News Broadcast*. https://eprints.lse.ac.uk/2945 /

Chouliaraki, L., & Fairclough, N. (2001). *Discourse in Late Modernity, Rethinking Critical Discourse Analysis.* Sage publishing.
Cohen, D. H. (2009). *Keeping an Open Mind and Having a Sense of Proportion as Virtues in Argumentation.* St Martin's Press.
Cole, D. (2003). *Enemy Aliens: Double Standards and Constitutional Freedoms in the War on Terrorism.* New Press.
Ditrych, O. (2014). *Training the Discourses of Terrorism: Identity, Geneology and State*. Palgrave, Macmillan.
Exposito, J. L. (2002). *Unholy War: Terror in The Name of God*. Oxford University Press.
Fairclough, N. (1989). *Language and Power*. Longman Group (UK) Ltd.
Fairclough, N. (1995). *Media Discourse.* Edward Arnold.
Fischer, A. (2004). *The Logic of Real Arguments*. Cambridge University Press.
Gartenstein-Ross, D. (2009). *The Strategic Challenge of Somalia's Al-Shabaab*. Middle East Quarterly.
Gartenstein-Ross, D. (2011). *Bin Laden's Legacy: Why We're Still Losing the War on Terror.* Hoboken.
Goodin, R. E. (2006). *What's W rong with Terrorism?* Cambridge: Polity Press
Halliday, M. A. K. (1978). *Language as Social Semiotic: The Social Interpretation of Language and Meaning.* Edward Arnold.
Hansen, S.J. (2013). *Al-Shabaab in Somalia: The History and Ideology of a Militant Islamic Group*. Oxford University Press.
Hoffman, B. (2006). *Inside Terrorism* (REV-Revised, 2). Columbia University Press. http://www.jstor.org/stable/10.7312/hoff12698
Houtlousser, P & Van Eemeren, F.H (1999). *Strategic Manoeuvring in Argumentative Discourse*. Discourse Studies, John Benjamins.
Igwebuke, E.E. (2018). *Discursive Strategies and Ideologies in Selected Newspaper Reports on the Nigerian-Cameroonian Bakasi Peninsula Border Conflict, 3*(2) 151-168. https://doi.org/10.1177/2057047317748500
Jackson, R. (2005). *Writing the War on Terrorism: Language, Politics and Counter-terrorism*. Manchester University Press
Jackson, R. (2016). *Routledge Handbook of Critical Terrorism*. Routledge.
Jackson, R., Breen-Smyth, M., & Gunning, J. (2009*). Critical Terrorism Studies: A New Research Agenda.* Routledge.
Jowett, G, & O'Donnell, V. (2006). *Propaganda and Persuasion.* SAGE.
Kimotho, S. G., & Nyarang'o, C. N. (2019). Role of social media in Terrorism Crisis Communication. *International Journal of Information Systems for Crisis Response and Management*, *11*(1), 65–82. https://doi.org/10.4018/ijiscram.2019010104
Lacquer, W. (2001). *The New Terrorism.* Phoenix Press.
Lawyer, F.W., Maurer, C., Wraith, G.C. (2014). *Model Theory and Topoi*. Springer.
Malashenko, A. (2017). *Terrorism as a Global Phenomenon.* DOC Research Institute. https://doc-research.org/2017/02/terrorism-global-phenomenon/
Maria, K. (2012).*Terrorism and the Growing Threat of Weapons of Mass Destruction: Al-Shabaab* GRIN Verlag, https://www.grin.com/document/230939.
Martin, G. (2003). *Understanding Terrorism: Challenges, Perceptions and Issues*. Sage Publications.
Martin, G. (2008). *Essentials of Terrorism: Concepts and Controverses*. Sage Publications Inc.
Michael, T., & Lars, H (2010). *Al-Shabaab: The Internationalization of Militant Islamism in Somalia and the Implications for Radicalization Processes in Europe*.www.justitsministeriet.dk
Norris, P., Kern, M., & Just, M. (2003). *Framing Terrorism*. New York: Routledge

Oando, S., & Achieng. S. (2021). An Indigenous African Framework for Counterterrorism: Decolonising Kenya's Approach to Countering "Al-Shabaab-ism", *Critical Studies on Terrorism*, *14*(3), 354-377, https://doi.org/10.1080/17539153.2021.1958182

Odhiambo, E.O.S., Maito, T.L., Kassilly, J., Chelumo, S., Onkware, K. and Oboka, W.A. (2013) Al-Shabaab Terrorists Propaganda & the Kenya Government Response. *International Journal of Humanities & Social Science*, *3* (7), 125-131. https://www.researchgate.net/publication/

Odhiambo, S. (2014). *Uchanganuzi wa Matini za Kigaidi Katika Gazeti la Taifa Leo. Muswada wa Uzamifu* (Phd): Maseno University.

Reah, D. (2002).*The Language of Newspapers*. Routledge.

Richardson, J. E. (2005). *(Mis) representinting Islam: The Racism and Rhetoric of British*. https://books.google.co.ke/books/about/Mis_representing_Islam.html?id=WanqiF2XULsC&redir_esc=y

Ross, J. I. (2006). *Political Terrorism: An Interdisciplinary Approach*. Peter Lang.

Rusell, M., & Tyler, L. (2010). *Al-Shabaab. Pittsburg.* University of Pittsburgh.

Schmid, A. (2004). Terrorism-the definitional problem. *Case Western Reserve Journal of International Law. Res*. *36*(2) 375. https://scholarlycommons.law.case.edu/jil/vol36/iss2/8

Schmid, D. (2008*). Natural born celebrities: Serial killers in American culture*. University of Chicago Press.

Taaliu, S. T. (2017) *Fighting Terrorism in Universities in Kenya*. Kenya School of Education and Social Sciences, University of Embu. https://doi: 10.4236/jss.2017.53018

Toomey, M., & Singleton, B. E. (2014). *The Post 9/11" Terrorism" Discourse and its Impact on Non-State Actors: A Comparative Study of the LTTE and Hamas*. State University.

Van Dijk, T. A. (1976). *Text and Context, Explorations in Semantics and Pragmatics of Discourse*. Longman

Van Dijk, T. A. (1988). *News as Discourse. Hillsdale*. Ealbaum Associates Publication.

Van Dijk, T. A. (2008). *Discourse and Context: A Sociocognitive Approach.* Cambridge University Press.

Van Dijk, T. A. (2008). *Discourse and Power: Contribution to Critical Discourse Studies*. Macmillan.

Walton, D. N. (2013). *Methods of Argumentation*. Cambridge University Press.

Walzer, M. (2004). *Arguing About War, New Haven and London*. Yale University Press.